

MATUMAINI PROG NO:2524

TITLE: WHAT GOD DESIRES FOR US

SUMMERY: KINAZUNGUMZIA KUHUSU KILE AMBACHO KILE MUNGU
ANACHOKITAMANI KWETU.

TEXT: WAEBRANIA 13:17-21.

MADA: MAPENZI YA MUNGU JUU YETU

.....

Tushukuru kwanza kabla ya kulianza somo la leo.

OMBI.... Uliyetukuka juu ya vyote,,Mungu Mkuu na tena Mshahuri wa ajabu uliyetuumba,,,tunakushukuru kwa sababu ya nafasi hii ambayo umetupatia ili kutufunulia kuhusiana na Mapenzi yako kwetu kama wanao,,, Fungua mioyo yetu ili tukaweze kukuelewa vyema. Ni kwa Yesu tumeomba, Amina.

Ni siku na zaidi mno nafasi nyingine ambayo Mungu wetu ametujaalia ili kujifunza kutoka Nenoni mwake. Ninayo imani ya kwamba,, unaendelea vyema. Karibu sana kwenye somo hili la leo ambalo tumelipatia Kichwa,,*Mapenzi ya Mungu juu Yetu.*

Kipindi hiki ni cha Matumaini kutoka TWR Kenya.

Somo ni kutoka kwenye Waebrania 13:17-21.

Kwa hitimisha fundisho leo,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo ufuatao.....

WIMBO:

Ni kweli kabisa ya kwamba Mungu yu Mwema kwetu na wema wake waonekana kote.....Asante sana Wana-msanii kwa huo mzuri tena zaidi kwamba Mungu yu Mwema.....

Mimi naitwa, Vincent Amara.

Mtu wangu,,,katika uwepo wangu ulimwengu,,nimegundua ya kwamba,,watu wengi humwabudu Mungu au miungu kwa sababu ya kuwa na hofu. Wengine huamini ya kwamba,,,,ni lazima wajukumike zaidi kiviao ili kupata kibali cha Mungu au kuepuka adhabu yake.

Bwana wetu Yesu Ukristo,,,mpendwa ni tofauti tena zaidi.

Nataka kukuhimiza hivi,,,Mungu wetu,,hataki tumkaribie kwa hofu ya adhabu, bali kwa imani, upendo, na uhusiano wa karibu naye. Kupitia kwa Mwanawe Yesu Kristo Bwana wetu, Yeye Mwenyewe ametufungulia njia ya kuwa na amani naye na kufurahia uwepo wake kila siku.

Tunapoingia katika kulichambua neno hili kwenye Waraka huu kwa Waebrania 13:17-21,,, tunaenda kuyaona mambo matatu makuu tena mno ambayo Mungu anatamani kuyaona katika maisha ya watoto wake.

Biblia inasema hivi;

17. Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; kwa maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa huzuni; maana hiyo haiwafai ninyi.

18. Tuombeeni; kwa maana tunaamini kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuishi kwa unyofu katika mambo yote.

19. Lakini nawasihi sana mfanye hivyo, ili nirudishwe kwenu upesi.

20. Basi Mungu wa amani, aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji mkuu wa kondoo, Bwana wetu Yesu, kwa damu ya agano la milele;

21. Akafanye ninyi wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yenu lile lipendezalo machoni pake, katika Yesu Kristo; utukufu una yeye milele na milele. Amina.

Kama ambavyo tumelisoma neno hili,,,Jambo la kwanza kabisa ambalo tunalipata ni kwamba,,, *Mungu wetu Anataka tuwe watiifu na pia wataratibu.*

Mpendwa,,,Mungu wetu amewaweka viongozi wa kiroho katika kanisa ili watufundishe, watuombee, na kutusaidia kukua katika imani.

Viongozi hao wanalo jukumu kuu tena zaidi mbele za Mungu kwa maana wanawajibika kwa ustawi wa kiroho wa waamini.

Kwa hivyo Mungu anatufundisha,,,kuwaheshimu viongozi wa kiroho,,,kuwa na roho ya unyenyekevu,,,kuwa tayari kujifunza,,,, n ahata kushirikiana katika maombi.

Mtume aliwaambia waamini hivi katika aya ya 18,, "Tuombeeni."

Rafiki yangu,,,hii inaonyesha ya kwamba hata viongozi wa kiroho wanahitaji maombi ya watu wa Mungu.

Maisha yenye utaratibu wa kiroho hujengwa kwa utii, unyenyekevu na zaidi sana maombi.

Jambo linalofuata ni kwamba,,,*Mungu Anataka tuwe na amani.*

Tukirejelea kwenye aya ya 20,,,Biblia inasema,, "Basi Mungu wa amani, aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji mkuu wa kondoo, Bwana wetu Yesu, kwa damu ya agano la milele;..."

Ndugu pamoja na dadangu,,,Mungu wetu ndiye chanzo cha amani ya kweli.Ulimwengu huu unaweza kukupatia starehe ya mda mfupi tuu, lakini amani ya kweli hutoka kwa Mungu pekee.

Amani hiyo ilipatikana kupitia kwa damu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Yesu alimwaga damu yake msalabani ili kutupatanisha na Mungu,,mpendwa.

Dhambi ilikuwa imetutenganisha na Mungu, lakini kwa kifo cha Yesu njia ya kurudi kwa Mungu ilifunguliwa.

Kupitia kwa ufufuo wa Bwana wetu Yesu Kristo ambaye yu hai,,tunaweza kuwa na uhakika wa wokovu na amani ya kweli.

Yesu katika Injili ya Yohana 14:27,,,Neno linatuambia kuwa,,Akasema hivi; "Amani yangu nawapa; si kama ulimwengu utoavyo."

Rafiki yangu,,Mungu wetu anatamani kila mwamini aishi katika amani hiyo kila siku.

Jambo la tatu na la mwisho kwa leo kutokana na fungu hili la neno ni kwamba,,,,Mungu wetu *Anataka tufikie ukamilifu wa Kiroho*

Katika aya ya 21 kutokana na somo hili leo,,,,,Biblia inasema ya kwamba...,

"Akafanye ninyi wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake."

Msikilizaji wangu,,,ukamilifu unaozungumziwa hapa bila shaka ni wa kukufanya ukomae katika maisha yako ya kiroho na kufanana zaidi na Kristo. Mungu wetu hufanya kazi hiyo ndani yetu tunapomruhusu kuyatawala yetu.

Mungu wetu hufanya kazi ndani yetu tunapomfungulia mioyo yetu.

Kwa kuifungulia mioyo hii kwake,,,bila shaka Yeye, hutufundisha,,hutubadilisha,,hutusafisha na hatimae kutujenga kiroho.

Ndugu na dadangu,,,nataka kukuchanua ya kwamba,,,mabadiliko ya kweli huanzia ndani ya moyo wako.

Kupitia Yesu Kristo,,,hakuna mwanadamu anayeweza kujifanya mkamilifu kwa nguvu zake mwenyewe. Bwana wetu Yesu Kristo ndiye anatufanya kuwa wakamilifu.

Yeye ndiye aliyeishi maisha matakatifu na makamilifu kabisa.

Tunapomtegemea Yesu kila siku, Mungu hutubadilisha hatua kwa hatua ili tufanane naye.

Na kwa kukamilisha,,tunapolitazama neno kutoka kwenye Waraka kwa

Waebrania 13:17-21,,tunajifunza kwamba Mungu anatamani mambo matatu muhimu katika maisha yetu.

Yaani,,,utaratibu na utii,,,amani ya kweli na hatimae,,,ukomavu na ukamilifu wa kiroho.

Rafiki yangu,,,mambo haya hayapatikani kwa nguvu za kibinadamu pekee,,,bali yanapatikana tunapomwamini Yesu Kristo na kumruhusu Mungu afanye kazi ndani mwetu.

Kadiri tunavyozidi kutembea pamoja na Kristo, ndivyo tunavyozidi kuwa watu ambao Mungu alikusudia tuwe.

'Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.

Hiki ni kifungu cha kukuhimiza popote ulipo mpendwa,,Wafilipi 2:13

Nakusihi Umkaribishe Kristo maishani mwako,,nawe bila shaka utaipata amani ya milele.

Ukifanya hivyo,,nizungumzie kwa anwani nitakayo kupa,,na nitakutafuta kwa mahimizo ya Kiroho.

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili kuhusiana na *Mapenzi ya Mungu juu Yetu.*

Kwa kweli tutalizingatia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu *Mapenzi ya Mungu juu Yetu.*

Tumeutoa kwenye waebrania 13:17-21

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,ni wimbo,,, nichapie hawa naye mtumishi Sarah Magesa

.....

WIMBO.....

Anasema ya kwamba Mungu nichapie hawa walio kinyume na mimi.Asante sana

our sister Sarah Magesa kwa wimbo huo mzuri.....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri